TEKNOLOJIA

# Dk. Kusiluka: Wataalamu TEHAMA tumieni ujuzi kwa maslahi ya taifa

**Na Romana Mallya,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, amewataka wataalamu wa TEHAMA serikalini kutumia ujuzi wao kwa maslahi ya nchi.

Amesema endapo ikitumika vibaya huleta athari kwa jamii, ikiwamo matumizi mabaya ya mitandao na uhalifu wa kimtandao.

Alitoa agizo hilo juzi jijini Arusha wakati akifungua Kikao Kazi cha Sita cha Serikali Mtandao (e-GA), kinachoendelea jijini hapa kwa muda wa siku tatu.

"Ni wajibu wenu wataalam mtumie taaluma zenu, ubunifu na maarifa kwa maslahi mapana ya taifa," alisema.

Balozi Dk. Kusiluka alisema anaeleza hayo kwa kuwa TEHAMA inaweza kutumika vibaya na kuhatarisha usalama na maslahi ya taifa.

Alisema katika nyakati hizi za mageuzi makubwa na ya kasi ya TEHAMA kumeshuhudiwa matumizi mabaya ya teknolojia ikiwamo kuharibu umoja na mshikamano wa jamii na uhalifu wa kimtandao. Hivyo, amehimiza wabuni vitu vinavyoleta maendeleo na kuhakikisha watu hawatumii vibaya mitandao.

Alisema ni muhimu wadau kuhakikisha wanaongoza watumiaji wa mitandao hasa vijana ambao baadhi yao wametekwa na Akili Unde (AI), ili watumie kwa vitu chanya badala ya hasi na kulinda maslahi, mila na desturi za taifa.

Kadhalika, alisema kutokana na kuongezeka changamoto ya usalama mtandaoni, matumizi ya *teknolojia* zinazochipukia, anaamini kupitia kikao kazi hicho, watajadili kwa kina namna ya kutumia teknolojia hizo kulinda maslahi ya taifa.

Pia, ameipongeza e-GA kupitia kituo chake cha Utafiti, Ubunifu na Uendelezaji wa Serikali Mtandao (eGOVRIDC), kwa juhudi za kuendeleza utafiti na bunifu za kidijitali, hasa katika teknolojia zinazoibukia.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi e-GA, Dk. Mussa Kissaka, alisema kikao hicho kimewakutanisha viongozi wa taasisi za umma, wataalamu wa TEHAMA, sekta binafsi na wadau wengine wa Serikali Mtandao kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kujadili mafanikio na changamoto.

Mkurugenzi Mkuu e-GA, mhandisi Benedict Ndomba, alisema mamlaka hiyo imeendelea kusimamia na kuratibu matumizi ya TEHAMA serikalini kwa kuzingatia Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019.



Alisema pia kuimarisha usimamizi wa miradi ya TEHAMA, uendeshaji wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (GOVNET) na kuongeza ufanisi wa ubadilishanaji taarifa kati ya taasisi za umma.

Kikao kazi hicho kimebebwa na kaulimbiu isemayo: 'Kuboresha utendaji wa serikali kwa kuimarisha utoaji wa huduma za umma kupitia mifumo salama na jumuishi serikali mtandao'.



MAENDELEO

# Mwigulu: Nchi ... uelekeo sahihi

**Na Mary Mosha,** SAME

WAZIRI Mkuu, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema nchi ipo kwenye uelekeo sahihi wa maendeleo, kwamba watendaji wa umma wanaofanyakazi kwa mazoezi na wazembe hawana nafasi katika serikali ya sasa.

Ameeleza hayo jana wilayani Same mkoani Kilimanjaro, wakati akipokea taarifa ya miradi ya barabara na mingine ya maendeleo ambayo haijakamilika licha ya fedha zake kutolewa tayari.

"Nimepewa taarifa kuhusu mradi wa barabara ambao haujakamilika. Nitahitaji maelezo ya kina kujua kwa nini haujakamilika, hasa kwenye maeneo ambayo fedha zilishatolewa," alisema.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya watumishi kusinzia katika utekelezaji wa majukumu yao na kusisitiza kuwa vitendo vya ubadhirifu wa fedha za umma havitavumiliwa.

"Kumekuwa na tabia ya kusinzia kwa baadhi ya watumishi. Kwenye ubadhirifu lazima watu wawajibike. Haya mambo ya uzembe na uvivu hayakubaliki, na sitayavumilia," alisema.

Waziri Mkuu alieleza kuwa watumishi watakaobainika kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo wanapaswa kuondolewa katika nafasi zao, ili kutoa nafasi kwa wenye uwezo wa kuwahudumia wananchi.

Alitolea mfano mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Suji-Gonjanza, akisema fedha zake zilitolewa tangu mwaka jana, lakini hadi sasa ujenzi haujaanza.

"Fedha za kujenga Kituo cha Afya Suji-Gonjanza zilifika tangu mwaka jana, lakini ujenzi haujaanza. Mheshimiwa Waziri fuatilia kujua tatizo ni nini," alisema.

Aidha, alieleza kuwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Same yenye vitanda 800 bado haujaanza, huku baadhi ya majengo yaliyojengwa yakionekana kuwa na nyufa.

Alisema pia madarasa saba katika eneo la Kihurio yameanguka yote, hali inayohitaji uchunguzi wa haraka ili kubaini chanzo cha tatizo hilo.

"TAKUKURU fuatilieni kujua nini ki-

naendelea k... aliagiza.

Dk. Nche... Wakala wa ... na Mijini (T... sha fedha zi... ya miradi z... na kuonya ... mabaya ya... siokuwa na...

Alisisitiz... zi sita ya ... hataki kus... sekondari ... matundu y...

"Ndani ... kusikia ku... ambazo h... vyoo. Mk... kuta hali h... alisema.

Pia aliwa...

J...

Simu: +25...
Fax: +255...
Barua Pe...
Tovuti: w...

1. Ndu... 19-2-... Mzig... Dod...
2. Gari...

Ure...
Up...
Kin...

3. Nji... Mo... sa...